**LEARNING BY EAR**

# "If a tree falls… - Deforestation in Africa"

**<u>EPISODE TEN: "A blessing"</u>**

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

**<u>List of characters EPISODE TEN:</u>**

**Narrator**

**SCENE1:** **Isi (m, 18)**

**INSERT:** **Isi (m, 18)** **Sesi (f, 18)**

**SCENE 2** **Akiki (f, 7)** **Sesi (f, 18)**

**SCEN E 3** **Talib (m, 20)** **Chief (m, 40)** **"Themba" (f, 30)** **Mulogo (m, 22)** **Group of Men/Women**

**SCENE 4** **Akiki (f, 7)** **Mother (f, 36)**

**SCENE 5** **Sesi (f, 18)** **Mother (f, 36)** **Akiki (f, 7)** **Isi (f, 38)**

**SCENE 6** **Mother (f, 36)** **Isi (m, 18)**

**SCENE 7** **Mulogo (m, 22)** **Chika (f, 18)** **Talib (m, 20)**

**SCENE 8** **Akiki (f, 7)**

**INTRO**

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha kumi cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Kwenye mchezo wetu huu tumeshuhudia jamii mbili zikianzisha shirika linaloitwa FARM – kundi shirikishi la usimamizi wa misitu. Mulogo ametambua kuwa ufumbuzi wa kienyeji wa matatizo ndio njia rahisi zaidi isiyo na gharamalakini anatamani sana kuanzisha mradi wa kijamii wa nishati mbadala. Lakini je ni jambo gani ambalo Akiki amekuwa akiliweka siri muda huo wote, ambalo linajulikana sasa? Jiunge nasi kusikiliza kipindi cha mwisho cha mchezo huu wa redio.

**Episode TEN: "A BLESSING."**

**1.MUSIC UP**

**Scene 1**

**2.ISI NARRATOR:** Miezi miwili imepita tangu siku nilipomuuliza Sesi swali lililozuwa kiwewe….

**3. INSERT WITH APPROPRIATE SAD MUSIC (OPTIONAL)**

**4.SESI: (soft whimper)** Hmmm

**5.ISI:** Ulimuona ? Sesi, kwa hisani yako. Ndugu yangu yu hai?

**6.SESI**: **(whimpers louder, clearly upset)** Hmmm

**7.ISI:** Ati? Unataka kunishika mkono? Ndio huu.

**8.SESI: (Whimpers)** Hmm

**9.ISI:** Unalia. Mbona unaupapasa mkono wangu? Sesi tafadhali**(starts sobbing)** Ndo sababu unanitizama hivyo? Ndivyo mkono wako unaashiria? Mungu wangu! Ndugu yangu! **(sobs uncontrollably)** Kato!

**10.SESI:** **WHIMPERING SOFTLY**

**11.SAD MUSIC UP AND FADE (OPTIONAL)**

**12.ISI NARRATOR:** …Uchungu ungalipo na Sesi hajaweza kuongea tena. Lakini majonzi ya mama yamenitanabahisha jambo: ninapaswa kujikurubisha zaidi naye. Ninapaswa kujikaza. Baba na kakangu Jamal... sitaki kukisia ikiwa wa hai au la. Vinginevyo mambo yakiwa kama ya Kato itakuwa pigo lisilovumilka. Nawajali sasa Sesi na Akiki. Ni wasiri sana. Pengine kwa kuwa wamepoteza kila kitu.

**13.MUSIC UP**

**<u>Scene 2</u>**

**<u>14.SFX Daytime ambience inside</u>**

**<u>15.DRAMATIC MUSIC UP</u>. HOLD UNDER.**

**<u>16.Sesi whimpers throughout scene.</u>**

**17.AKIKI:** Sesi, huwezi kumwambia yeyote….
Unadhani itakuwa siri mpaka lini? Na unajua nani ndiye baba… lazima umjulishe Ma… na Isi…. Ni vibaya ikiwa hawataambiwa. .. Tafadhali Sesi waambie… hivi karibuni…leo…….sasa …..

**<u>18.DRAMATIC MUSIC UP AND OUT</u>**

**Scene 3**

**19. SFX Daytime ambience outside**

**Women/men and boys voices**

**20.TALIB:** Wakazi wa kambi ya Dovani. Asanteni sana kwa kuhudhuria mkutano wa leo wa shirika letu la FARM. Nafurahi kuona kwamba wengi wetu mmefika. Si rahisi kwa watu wenye familia zao, kuhangaikia maisha na kisha wapate fursa ya kuhudhuria vikao hivi.

**( VOICES OF APPROVAL)**

Napenda kusema wazi – hakuna faida yoyote ya kifedha mtu anayopata kwa kujiunga na FARM. Lakini kumbukeni- mnapata uzoefu wa kusimamia misitu, stadi za usimamizi, sheria za kimsingi kuhusu mali, haki za kisheria na mbinu za kushauriana. Watu wengine wanapaswa kulipa karo za chuo ili wapate maarifa kama hayo! **(Laughter)** Mtahitimu bila kugharamika! Mnaweza kuwa wajuzi wa taaluma ya kilimo kinachohusisha upandaji miti, wataalamu wa uhanuai, wajuzi wa habari za miti na mimea, thamani ya magome yake, mbegu na matunda.. Na yote hayo yatatupatia kipato. Chifu Apaloo! Tafadhali tuambie hatua yetu nyingine ni ipi. Umelifikiria suala hilo kwa muda. Kisha wengineo watachangia.

**22.CHIEF APALOO:** Asante Talib. Una kipaji cha ajabu cha uongozi! **(Applause)**

Na umewahamasisha vijana hapa kuelewa mabadiliko ya hali ya hewa na jinsi ya kuishi bila kuharibu mazingira. Kwa upande wangu, ningependa kupata watu wanaojitolea kunisaidia kutengeneza majiko hapa kambini kisha tuyauze-naam tuyauzie nyumba zilizopo hapa. Kama utapata moja utalitunza vizuri.

**24.THEMBA:** Bei kiasi gani Chifu? **(Laughter)**

**25.CHIEF APALOO:** Hapa kambini tunaweza tu kubadilishana bidhaa – mboga na maziwa, njugu na matunda kwa jiko moja. Lakini tukirejea makwetu tutajiunga na mradi wa mkopo wa FARM. Bila shaka tunahitaji msaada wa mfadhili kwanza. Tutakapoanza kupata fedha tutapata wafadhili kisha tulipe mikopo yetu.

**26.MULOGO:** Hayo si mambo mageni! Wengine wameshayapitia na jukumu letu sisi ni kujifunza na kujiimarisha zaidi. **(Applause)**

Mfumo wa mikopo wa FARM utakuweko kwa muda.

**27.THEMBA:** Kwani ni mpango wa kifamilia? **(Embarrassed hush)**

**28.MULOGO:** Utakuwa hivyo ikiwa hutajihusishai!

**29.CHIEFAPALOO:** Ni jukumu langu na uchifu wangu kuwahudumia nyote.

**30.MULOGO:** Lakini ni jukumu lenu nyote kutoruhusu ulaghai wa aina yoyote, iwe kupendeleana kijamaa au ufisadi wa aina nyingine yoyote. Mtawapigia viongozi kura na wakishindwa kutekeleza majukumu yao mnawaondoa. Na ili kufanya hivyo, inawabidi mjihusishe! Hiyo ndio hali ya demokrasia!

**<u>31.MUSIC UP AND FADE ON APPROVING MURMUR OF VOICES</u>**

**Scene 4 34. SFX daytime ambience inside**

**32.AKIKI:** Ma? Sesi ana jambo anataka kukwambia.

**33.MOTHER:** Sesi? Anaongea?

**34.AKIKI:** La. Lakini anaweza kuashiria kwa mikono yake.

**35.SESI:** **soft whimpering**

**37.MOTHER:** Sesi? Una nini mwanangu?

**38.SESI:** **soft whimpering**

**39.MOTHER:** Unataka nikuguse? Wapi? Hapa?

**40.AKIKI:** Unahisi kitu chochote ma?

**41.SESI:** **whimpers more urgently**

**42.MOTHER:** Nini? Kuna tatizo gani?

**43.AKIKI:** Ebu tazama mahali anapoweka mkono wako.

**44.MOTHER:** Ai Sesi! Wewe ni …Wewe ni mjamzito!

**45.SESI:** **Whimpers softly**

**46.MOTHER:** Ati? Lakini vipi? Wapi? Nani babake mtoto?

**47.AKIKI:** Ma. Hujamwona jinsi Sesi anavyohamaki pindi Isi anapoingia chumbani? Anajua ma.

**48.MOTHER:** Anajua nini? Isi? Unataka kunambia Isi ndiye aliyefanya haya?

**49.SESI:** **more agitated whimpering**

**50.AKIKI:** Hapana Ma. Si Isi. Ni nduguye pacha.

**51.MOTHER:** Kato? Lini? vipi?

**52.AKIKI:** Walikuwa wakijificha katika mti wa mbuyu ule niliompata Sesi. Kato …Kato ndiye baba, ma.

**53.MOTHER: (Begins to sob)** Ati nini? Na yuko wapi sasa?

**54.SESI: sobbing/whimpering**

**55.AKIKI:** Tazama. Sesi amenichorea mchoro huu ma.

**<u>56.SFX PAPER/SESI WHIMPERING</u>**

**57.MOTHER:** Huyu si mtu anayeuawa na wanajeshi?

**58.AKIKI:** Naam ma. Kato aliuawa. Sesi alijificha kwenye mbuyu. Kama yule mzee ulionipa hadithi yake. Na mtoto …

**59.MOTHER: (sniffing, quietly, in awe)** …ni mjukuu wangu. Mungu wangu!

**<u>60. MUSIC UP</u>**

**Scene 5**

**61. SFX. EVENING AMBIENCE OUTSIDE**

**62.MULOGO:** Chika! Unaoneka umechoka. Keti!

**63.CHIKA:** Nimesaidia kuzalisha mtoto wangu wa kwanza! Ni mtoto wa Kato! Sesi alilitaja jina la Kato uchungu ulipomzidi alipokuwa akijifungua, lakini nafuu ameweza kuzungumza tena Mulogo! Hivi sasa Sesi anaweza kuzungumza! Ajabu hiyo!

**64.MULOGO:** Shabashi! Mustakabali wako ni mzuri! Kweli Chika!

**65. SFX: KISSING**

**66.CHIKA:** Mama Kipko amefurahia kwamba Sesi amejifungua salama. Wanataka kumuita mtoto huyo wa kiume Buyu kwa sababu ya mtu huo wa mbuyu uliomwokoa Sesi.

**67.TALIB (Running over)** Chika! Nimezipata habari. Habari za kufurahisha. Habari nyingine za kuchangamsha pia zimetufikia. Chifu Kipko na Jamal watakuja kwa lori litakalofika hapa kesho jioni. Nimeipata pepesi jioni hii. Babake Isi na kakake wangali hai!

**68.SILENCE / MUSIC UP**

**Scene 6**

**69b. SFX OUT IN THE FIELDS**

**70.AKIKI:** Ai Isi! Tunapaswa kusherehekea!

**71.ISI:** Ninataka kusherehekea pia! Mtoto huyo anaashiria taswira ya Kato ndugu yangu. Kato yu hai! Na kesho usiku katika kambi ya Dovani tutawasha moto mkubwa tusherehekee kwa kucheza ngoma!

**<u>72.KIROKO MOOS</u>**

**73.AKIKI:** Ai Kiroko!

**74.ISI:** Je unakumbuka kitandawili nilichokuuliza? Mti unapoanguka na hakuna mtu karibu kusikia, je unatoa sauti yoyote?

**75.AKIKI:** Sina jibu! Wewe unafikiri nini?

**76.ISI:** Naam …Nadhani kama hakuna wanadamu waliobaki katika dunia hii kusikia sauti, hapo inawezekana, kwa kuwa ni kama kwamba hakuna sauti. Nani ambaye angesema kama amesikia sauti hiyo?

**<u>77.KIROKO MOOS SOFTLY</u>**

**78.AKIKI: (Laughing)** Jibu lako hilo! Kiroko angelisikia!

**79.ISI: (Laughing)** Ah! Naam! Bila shaka – angehisi athari ya mti huo ukianguka kwa kuwa hakungekuwa na maeneo ya malisho, majangwa tu yaliyojaa miti iliyokauka.

**80.AKIKI:** Ni lazima tuache kuangamiza miti yetu mizuri!

| | |
|---|---|
| **81.ISI:** | Kweli, Akiki! Vita hivi vikimalizika, tutakuwa na vita vingine vikubwa vya kukabiliana na ongezeko la joto duniani, maziwa yaliyokauka na milima isiyokuwa na miti. |

**82.KIROKO MOOS**

| | |
|---|---|
| **83.AKIKI:** | Ni lazima tuhifadhi misitu! Kwa sababu niliwahi kumkuta dadangu msituni. Mtoto wake alizaliwa msituni. |
| **84.ISI:** | Na sote tutarejea kwenye misitu na mashamba yetu na tujenge jamii mpya. Njoo Akiki! Kiroko njoo. Hatimaye nishajua tunachotakiwa kufanya! |
| **85.AKIKI:** | Njoo Kiroko! **(Clicks her tongue several times to move the cow.)** |

**86. Cow moos**

**87. FADE INTO HAPPIER MUSIC (HOLD UNDER CREDITS)**

**OUTRO.**

Umekuwa ukisikiliza kipindi cha mwisho katika mfululizo wetu wa vipindi vya mchezo wa redio unaoitwa: "Mti unapoanguka...", ulioandikwa na Romie Singh......(MORE CREDITS?)

Tumeonyesha jinsi jamii za mashambani zinavyoweza kushirikiana kusimamia rasilimali kama vile misitu, mashamba, maeneo ya malisho, na hata maji.
Ili kuiokoa dunia yetu, tunapaswa kukabiliana vilivyo na tatizo la uharibifu wa misitu na pia kudhibiti ongezeko la joto. Bara la Afrika lina jukumu muhimu la kuhifadhi misitu yake na kuanzisha mbinu za kilimo ambazo zitapunguza gesi za sumu zinazochafua mazingira.

Tunatumai umevifurahia vipindi hivi. Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri!

**END OF EPISODE TEN**